# Maumbo ya Fasihi Simulizi katika Mashairi Andishi Teule ya Kiswahili

*Miruka Frida Akinyi*[1] na *Florence Indede*[2]
[1]*Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Jaramogi Oginga Odinga, Kenya*
[2]*Chuo Kikuu cha Maseno, Kenya*

**Ikisiri**

**Asili ya mashairi ya Kiswahili ni nyimbo simulizi za jamii za Afrika mashariki. Pamoja na vipera vingine vya fasihi simulizi, nyimbo huingiliana katika kujenga mashairi andishi ya Kiswahili. Hata hivyo baadhi ya wasomi katika viwango anuwai wamepuuza fasihi simulizi na kuichukulia kama utanzu sahili wenye thamani duni huku ushairi ukidhukuriwa kama utanzu tata. Makala hii inatalii maumbo ya fasihi simulizi katika mashairi andishi ya Kiswahili ili kuonyesha thamani ya fasihi simulizi katika kujenga mashairi andishi. Data sekondari ilikusanywa kwa kudurusu diwani tatu zilizoteuliwa kimaksudi kuwakilisha vipindi vitatu katika historia ya ushairi mathalani Utenzi wa Fumo Liyongo (Kijumwa, 1964) kuwakilisha kipindi cha urasimi, diwani ya Sauti ya dhiki (Abdalla, 1973) kuwakilisha kipindi cha urasimi mpya na diwani ya Kichomi (Kezilahabi, 1974) katika awamu ya sasa. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa mtindo wa uchanganuzi wa matini. Uchunguzi ulionyesha kuwa maumbo manne makuu ya fasihi simulizi hujenga mashairi andishi ya Kiswahili. Matokeo haya ni muhimu kwa kuonyesha nafasi ya fasihi simulizi katika mashairi andishi na hivyo kuonyesha namna fasihi simulizi inavyoweza kutumika kusahilisha uchambuzi wa mashairi.**

Maneno Muhimu: *Fasihi Simulizi, Mashairi, Maumbo*

## Utangulizi

Ushairi hujitokeza katika awamu nne kihistoria ingawa tatu kati yazo ndizo muhimu. Mathalan vipindi vya urasimi, urasimi mpya na usasa (King'ei & Kemoli, 2001). Katika awamu hizi mashairi yamekua kutoka maumbo sahili ya nyimbo hadi maumbo ya kiarudhi na hatimaye maumbo tata yaliyo huru. Licha ya hali hii majaribio machache mno yamefanywa kuonyesha uhusiano wa tanzu za ushairi na fasihi simulizi. Hivyo, fasihi simulizi huchukuliwa kama utanzu duni huku ushairi ukipewa thamani na kuchukuliwa kuwa tata. Ni katika msingi huu ambapo makala hii inashughulikia maumbo ya fasihi simulizi katika mashairi andishi ya Kiswahili.

## Mbinu za Utafiti

Uchunguzi ulitumia muundo elezi ambao huazimia kueleza hali jinsi ilivyo kwa kuhusisha ukusanyaji data, uainishaji, uchanganuzi, ulinganishi na ufasiri wa data (Kerlinger, 1969 katika Kombo & Tromp, 2006). Matini tatu zilizowakilisha vipindi vitatu kihistoria zililengwa, mathalani: *Utenzi wa Fumo Liyongo* ( Kijumwa, 1913); *Diwani ya Sauti ya dhiki* (Abdalla, 1973) na *Diwani ya Kichomi* (Kezilahabi, 1974). Data zilikusanywa maktabani kwa kudurusu maandishi kutumia jedwali la matukio. Uchanganuzi kisifa ulifanywa kwa uchanganuzi wa matini kihakiki. Data iliyochanganuliwa ilifasiriwa na kuwekwa kwenye mpangilio huku ikihusishwa na malengo na nadharia ya utafiti. Uwasilishaji ulifanywa kwa maelezo katika aya mbalimbali.

## Maumbo ya Fasihi Simulizi katika Ushairi wa Kiswahili

Suala la maumbo ya fasihi simulizi katika mashairi andishi ya Kiswahili linadhihirika katika dhana ya ushairi kama inavyoshughulikiwa na wataalam mbalimbali. Tapo la wanamapokeo limesisitiza sifa za ushairi kama: sanaa ya vina na urari wa mizani, lugha ya mkato, lugha nzito yenye kunata na kuimbika kwa shairi. Mnyampala (1965) kwa mfano anaeleza kuwa ushairi umejengwa kwa maneno ya hekima na sanaa ya vina, mizani na lugha ya mkato. Naye Abedi (1954:1) anasema, shairi au utenzi ni wimbo, hivyo kama shairi haliimbiki halina maana. Kadhalika Roberts (1972) anafafanua ushairi kama sanaa ya vina inayopambanuliwa kama nyimbo, mashairi na tenzi. Licha ya kusisitiza vina na mizani, wanamapokeo hawakosi kutaja maumbo ya fasihi simulizi kama nyimbo, mashairi na tenzi.

Wanamapinduzi kwa upande mwingine wanasisitiza lugha ya mdundo na ya mkato, yenye taswira na maudhui. Njogu & Chimerah (2007) wakimnukuu Topan wanasema, shairi ni utungo unaoeleza hisia za ndani kwa mpangilio fulani wa maneno. Naye Kezilahabi katika makala "Ushairi wa mapokeo na wakati ujao" anasema ushairi ni tukio, hali au wazo ambalo limeonyeshwa kwetu kutokana na upangaji mzuri wa maneno fasaha yenye mizani kwa ufupi, ili kuonyesha ukweli fulani wa maisha. Kwa upande mwingine, Mulokozi & Kahigi (1979) wanasema ushairi ni sanaa inayopambanuliwa kwa mpangilio maalumu wa maneno fasaha na yenye muwala, kwa lugha ya mkato, picha au sitiari, katika usemi, maandishi au mahadhi ya wimbo, ili kueleza tukio au hisi fulani kuhusu maisha kwa njia inayogusa moyo. Maumbo simulizi yametajwa katika fasili za pande zote.

Asili ya mashairi pia imehusishwa na methali (Knappert, 1979; Tylor, 1963). Kwa mujibu wa Knappert, sababu iliyowapa Waswahili hamu ya kutunga mashairi ni wingi wa methali ambazo zilifuata mapigo, na mapigo haya ndiyo yalizua mashairi. Asili ya mashairi basi inahusishwa na maumbo ya fasihi simulizi kama methali na nyimbo. Makala hii inabainisha maumbo mengine ya fasihi simulizi yanayodhihirika katika mashairi andishi ya Kiswahili.

Wanamapokeo pia wanataja maumbo simulizi. Abedi (1954) kwa mfano anataja wimbo na kuimbika kwa shairi. Naye Roberts (1972) anasema kuwa shairi au utenzi ni sanaa ya vina inayojibainisha kama tenzi, mashairi au nyimbo. Kando na nyimbo,

maumbo mengine yaliyotajwa ni tenzi na shairi. Naye Ntaragwi (2004) anaongeza maumbo mengine kama vile wajiwaji, hamziya na tumbuizo. Kwa mujibu wa Ntaragwi, shairi ni mojawapo ya tanzu za mashairi ilhali ushairi ni namna ya kutunga shairi au mashairi na tunapata tungo kama vile tenzi, nyimbo, wajiwaji, hamziya, tumbuizo na shairi. Kutokana na mawazo haya tunaona mpaka baina ya mashairi na fasihi simulizi kwani maumbo ya fasihi simulizi yanatajwa katika ushairi, dhana ambayo kwa mujibu wa Ntaragwi ni namna ya kutunga mashairi. Hivyo basi ina maana kuwa wanapotunga mashairi watunzi huweza kutumia maumbo ya fasihi simulizi. Makala hii inaangazia maumbo simulizi katika mashairi andishi kwa msingi wa dhana kuwa ushairi andishi ni muingiliano wa maumbo ya fasihi simulizi.

Kutokana na makala hizi, ni bayana kuwa ushairi umetokana na nyimbo. Vilevile fasili mbalimbali zinataja maumbo ya fasihi simulizi. Hata hivyo tofauti kati ya tanzu hizi zimesababisha ushairi andishi kuchukuliwa kama utanzu tata huku fasihi simulizi ikichukuliwa kama utanzu sahili. Kuchunguza maumbo simulizi katika mashairi andishi kutatoa msingi wa kuchunguza na kuelewa mashairi andishi kwa msingi wa fasihi simulizi.

## Maumbo ya Fasihi Simulizi

Maumbo manne makuu ya fasihi simulizi yalidhihirika katika matini zilizochunguzwa.

### Hadithi

Hadithi ni masimulizi yanayotumia lugha ya mjazo na mtiririko wake huwa mwepesi au sahili (Wamitila, 2010:25). Hadithi hubainika kwa matumizi ya sifa kadhaa kama vile matumizi ya lugha ya nathari, matumizi ya fomula za kisimulizi, mianzo yenye maneno ya kuvutia, na ploti yenye mtiririko wa moja kwa moja. Vipera vitatu vya hadithi vilivyodhihirika ni hurafa, mighani na "hadithi nyingine" au "hadithi huria" ambazo kwa mujibu wa makala hii ni hadithi zisizotosheleza sifa za utanzu maalum wa hadithi ila huonyesha mitindo ya kisimulizi. Maumbo ya hadithi yanayodhihirika ni:

### Mighani

Mighani ni hadithi zinazozunguka kwenye matendo ya mashujaa wa jamii fulani (Wamitila, 2010:77). *Utenzi wa Fumo Liyongo* ni mughani. Wafula & Njogu (2007:40) wakizungumzia sifa za fasihi ya Kiswahili katika misingi ya Kirasimi wanasema, masimulizi marefu kama vile tenzi yana mwanzo, kati na mwisho. Katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*, utangulizi unaashiria mwanzo wa hadithi:

Bismillahi nabutadi
Kwa ina la Muhammadi
nandikie auladi
nyuma watakaokuya

Unipe wino mweusi

Na ya shamu karatasi
na kalamu ya unyasi
nipate kuyandikia

Na kibao cha fadhari
nipijie misitari
khati zende kwa uzuri
zifuwate moya ndiya

Hadithi niwandikiye
ya ajabu musikiye
yalojiri amriye
mupate kufahamiya

Utungo huu unaanza kwa bismillahi, kuomba wino na kalamu na mtunzi kutaja kuwa kipera kinachowasilishwa ni hadithi. Katika dondoo hili sauti ya msimulizi inabainika anapotumia nasfi ya kwanza. Katika ubeti wa tano uliodokezwa anatueleza hadithi ya Liyongo kwa utungo. Katika hitimisho, mtunzi anaomba dua za mwenyezi mungu (beti, 228-232). Zifuatazo kwa mfano ni beti za 228 na 229:

Tumeziye kukhitimu
Hapo ndio wasalamu
ilahi tatukirimu
kwa Baraka na afiya

Rabi tatusahiliya
na uzito wa duniya
tena tatujaaliya
kuwa njema yetu niya

Akimnukuu Keen (2015), Foster (1927) anaeleza kuwa sifa ya pili ya masimulizi ni ubainishaji wa wahusika. Mhusika Liyongo anabainishwa kwa mfanano katika kauli: ‘Kimo kawa mtukufu, mpana sana mrefu’ na ‘Ni mwanamume swahili, kama simba una zihi’ (beti 7, 14-16)

Sifa ya tatu ya muundo wa masimulizi kwa mujibu wa Foster ni ploti (Keen, 2015:74-75). Foster anaeleza kuwa ploti ni masimulizi ya matukio kisababishi. Kwa mujibu wa M’Ngaruthi (2008:50), ploti huonyesha muoano wa matukio yanayojenga hadithi. Hadithi ya Liyongo inajitokeza kwa ploti yenye sehemu tatu. Kwanza, tunapewa maelezo kuhusu Liyongo, sifa zake na uhusiano wake na Wagalla. Kilele cha usimulizi kinabainika katika mgogoro unaoanza na fitina kumhusu Liyongo ambavyo vinasababisha uamuzi wa kumuua. Haya yanabainika katika ubeti wa 49. Kisha kuna majaribio ya kumuua Liyongo yanayosimuliwa kwa hatua zinazodhihirika kama hadithi ndani ya hadithi. Mathalan: ‘Karamu ya kikoa’ ambapo walitarajiwa kula makoma na ifikapo zamu ya Liyongo auwawe (beti 58, 59). Mpango huu hata hivyo haufanikiwi. Baadaye wanaandaa ‘densi ya mwao’ ambapo Liyongo anakamatwa na kutiwa gerezani kisha uamuzi unatolewa kuwa auawe. Tatu, tunapata ufumbuzi au sehemu ya mwisho ambapo mwanawe Liyongo anashawishika na kukubali kuchunguza

siri ya maisha ya babake. Anamuuliza babake kile kinachoweza kumuua. Anapopata habari hii anampelekea mfalme ambaye anapata suluhu ya haja yake. Huu unakuwa utatuzi wa mgogoro hadithini. Mwishowe mwanawe Liyongo anamuua babake kwa kumdunga msumari wa shaba kitovuni (ubeti 179). Tukio la mwisho ni kifo cha Liyongo kinachotokea kisimani. Utenzi huu basi ni hadithi ya kishujaa. Hivyo basi kipindi cha urasimi kinadhihirisha uwepo wa mighani.

### Hurafa

Hizi ni hadithi au ngano zenye wahusika wanyama wanaowakilisha tabia za watu (Ngure, 2003:95) Baadhi ya wahusika huweza kuwa vitu visivyokuwa na uhai (M'Ngaruthi, 2008:47). Katika *Diwani ya Kichomi,* mashairi 'Jinamizi' (uk.1) na 'Hadithi ya Mzee' ni hurafa. Shairi 'Jinamizi' linasimulia harakati za kupigania uhuru. Mtunzi anaeleza kisa cha ukoloni unaoendelezwa na askari wazungu (watu weupe) na Waafrika (watu weusi). Wahusika ni wanyama (samaki) ambao kwa kawaida hupatikana katika hurafa au ngano za wanyama. Matumizi ya nyakati zilizopita katika utangulizi yanadhihirisha mtindo wa masimulizi.

Katika shairi 'Hadithi ya Mzee', mhusika Babu anasimulia hadithi ya Nzige. Ni siku ya Jumapili na kila mtu amekwenda kusali.Watoto wamemzunguka mzee. Wanamwambia:

"Tusimulie hadithi!
Hadithi tusimulie!
Babu tusimulie!'' ub.1

Masimulizi yanaanza katika ubeti wa nne:

"Kwanza zilikuwa habari
Habari zisizoaminika
Kwamba huko pwani
Kumefika wadudu… ub. 4

Kezilahabi katika shairi hili anasimulia kimafumbo kisa cha wakoloni walioparamia bara la Afrika na hatimaye kufukuzwa na Waafrika baada ya kujinyakulia uhuru. Anasimulia harakati za ukoloni, mivutano kati ya wakoloni na wenyeji na hatimaye kushindwa kwa wakoloni. Hatua hizo tatu zinajenga msuko wa hadithi wenye sehemu tatu. Mwisho wa hadithi unaashiriwa na kauli "Huo ndio mwisho Mwisho wa hadithi yangu". Vipengele simulizi katika hadithi hii ni msimulizi (Babu), hadhira (watoto), mandhari ya kiwakati (siku ya Jumapili) na pahala maalum pa kutambia (watoto wameketi na kumzunguka mzee). Hurafa hizi zimedhihirika katika diwani ya *Kichomi* inayowakilisha kipindi cha Usasa.

### Hadithi Huria

Kwa mujibu wa makala hii hadithi huria ni tungo zenye matumizi ya mitindo ya kisimulizi ingawa haziwezi kuainishwa kama maumbo maalum ya hadithi kwa kukosa sifa tambulishi za maumbo hayo. Katika *Diwani ya Sauti ya Dhiki*, shairi '*Mja si*

*mwema*' (uk. 34) lina vipengele vya masimulizi kama vile utangulizi na ploti zinazobainika wazi. Ufuatao ni ubeti wa kwanza:

| | | |
|---|---|---|
| Mkono inuka | inuka hima | twaa kalamu |
| Upate yandika | kwa khati njema | hino nudhumu |
| Ipate someka | wenye kusoma | waifahamu |
| Wapate yashika | na kuyapima | yaliyo humu |

Ubeti huu ni utangulizi kama katika tenzi za Kiswahili. Unaanza kwa bismillahi, kuomba kalamu, wino na karatasi kisha kuirai hadhira kutega sikio kwa ujumbe utakaotolewa. Katika mloto wa ubeti wa pili, mshairi anasema: "Na mimi naanza kisa chenyewe cha mlimwengu". Shairi '*Telezi*' (uk. 24) ni masimulizi kuhusu mvua kuu iliyonyesha na kusababisha dhiki kwa waja. Mitindo miwili ya usimulizi wa nafsi ya kwanza na usimulizi wa nafsi ya pili imetumika katika hadithi hii.

Shairi '*Ukucha wa mbwa*' (uk.25) katika diwani ya *Kichomi* linasimulia kisa cha mama mjane kipofu ambaye anamrithisha mwanawe Amina ukucha wa mbwa. Mshororo wa kwanza, 'Palikuwa na mama mmoja' unaashiria mwanzo wa masimulizi. Mshairi anatumia masimulizi sahili kwa mtindo wa nafsi ya tatu. Shairi linawasilisha kisa cha mama mjane, kipofu na masikini ambaye maisha yake yanaongozwa na 'ukucha wa mbwa' ambao kwake ni 'dawa ya ulimwengu.' Hata hivyo ukucha huu hatimaye unammaliza pamoja na jamaa zake.

Katika shairi '*Hadithi ya kitoto'* (uk.42) kuna muktadha halisi wa tamaduni za Kiafrika ambapo hadithi zilitekeleza wajibu wa kuburudisha na kuelimisha hususan baada ya kazi. Utangulizi unatoa maelezo ya mandhari:

"Nipo hapa, nimekaa, mgongo upinde,
Nikiyanung'unikia mawingu ya mashariki
Nikiota moto ambao naomba
Usizimike mpaka kesho asubuhi…" (ub.1)

Dondoo hili kutoka ubeti wa kwanza linaonyesha mandhari halisi ya kutamba hadithi. Ubeti wa pili unaonyesha kuwa hadithi zinazotambwa ni ngano, 'zenye uongo lakini za kweli'. Mwanzoni, usimulizi wa nafsi ya kwanza unamtambua msimulizi. Baadaye hadithi inapoanza, usimulizi wa nafsi ya tatu unatumika. Katika ubeti unaofwata wajukuu wanamsihi msimulizi kuwasimulia hadithi. Huu ni mwanzo wa hadithi unaopewa muundo wa beti za mashairi. Mshororo wa kwanza wa ubeti huu "Palikuwa na mama mmoja", unathibitisha kuwa utungo huu ni hadithi. Mtindo huu pia unatumika katika '*Hadithi ya Mzee*' (uk.69). Katika mashairi haya sifa bainifu za fasihi simulizi za utendaji na mahala zinadhihirika. Mashairi mengine yenye maumbo simulizi ni *'Upepo wa wakati' (*uk.4), '*Uvuaji wa Samaki Victoria*' (uk.9) na '*Mto Wa Haki'* (uk.17).

Hadithi huria zinatoa mchango wa kipekee katika wasilisho hili kwani hamna hadithi za fasihi simulizi zinazoitwa hadithi huria.

## Maigizo

Neno maigizo linatokana na kitenzi 'iga', yaani tenda jambo kama atendavyo mwingine (M'Ngaruthi, 2008:08). Kwa mujibu wa Wamitila (2010:99), maigizo ni mpangilio wa maneno ambayo huambatana na utendaji wa wahusika ambao huiga mambo yanayopatikana na jinsi yanavyoonekana katika jamii. Vipera vya maigizo vinavyojitokeza katika ushairi ni mazungumzo, ngonjera, mawaidha na ngoma. Maumbo haya yanadhihirika katika mihula yote mitatu. Sifa mbalimbali katika mashairi yaliyochunguzwa zinasawiri utanzu wa maigizo. Katika shairi '*Dakika kumi na tano za uzalendo'* kuna maelekezo ya jukwaani, matumizi ya maleba na hadhira. Ifuatayo ni mifano ya maelekezo:

i. *Anaingia Mtangazaji amevaa kanzu, shuka nyeupe begani na kilemba cha taulo* (uk. 51).
ii. (*Anaingia kijana kutoka kushoto na mzee kutoka kulia. Wanakutana katikati, mzee anataka kupita)* uk.52.

Baadhi ya maelekezo yanaonyesha kuwepo kwa hadhira ambao ni wasikilizaji.

## Mazungumzo

Mazungumzo ni maongezi ya kimajibizano yanayotokea baina ya watu wawili au zaidi (Wamitila, 2010:208). Katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*, majibizano yanatokea baina ya makundi mbalimbali. Katika beti za 88-94, kuna mazungumzo baina ya makundi manne kuhusu kuuawa kwa Liyongo na jinsi ambavyo mpango huo ungetekelezwa. Kundi la kwanza linakataa kushiriki kwenye mpango wa mauaji ya Liyongo. Wao wanajitenga (ub. 88). Kundi la pili linadai kuwa Liyongo ndiye mtetezi kwa hivyo asiuwawe (Ub.89). Kundi la tatu linapendekeza kuwa Liyongo afanywe kuwa amiri vitani ili kukitokea vita afe vitani nao waepuke lawama ya kumuua (ub. 90). Nalo kundi la nne linakosa msimamo (ub. 91). Hata hivyo, Sultani mwenye mpango wa kutekeleza mauaji anaonelea kuwa ni heri kumuua kwani kumuacha ni hatari kwani angempokonya ufalme wake. Kundi la mwisho ni kundi la jamaa zake ambalo linaunga mkono shauri la kuuwawa kwa Liyongo (ub 93). Hali hii ni ithibati ya kauli ya M'Ngaruthi (2008) kuwa mazungumzo hayatokei tu baina ya watu binafsi bali pia baina ya makundi mbalimbali. Makundi matano yanahusika katika mazungumzo haya. Mifano mingine ni mazungumzo baina ya Kitwana na Liyongo (beti 95-99), Sultani na Liyongo kupitia kwa Kitwana na Liyongo na mwanawe kuhusu 'kile kimuuacho babake (beti 135-145).

Katika *Diwani ya Kichomi* majibizano yanajitokeza katika shairi *'Hadithi ya kitoto'* (uk.42). Mandhari ya mwanzo wa hadithi yanasawiri msimulizi na wajukuu wanaomsihi kuwasimulia hadithi. Katika hadithi inayosimuliwa pia kuna wahusika wanaojibizana. Kwa mfano katika beti za 18 -20 kuna majibizano baina ya Kanana na mumewe anayeitwa Katili. Kadhalika mtindo huo wa mazungumzo unatumika katika shairi *'Hadithi ya Mzee'* (uk.69) kama kitangulizi. Ufuatao ni mwanzo wa shairi hili:

Ilikuwa siku ya Jumapili
Wakatikila mtu

Alikuwa amekwenda kusali
Watoto walipomzunguka
Mzee na kumwambia
"Tusimulie hadithi!
Hadithi tusimulie!
Babu tusimulie " ub. 1

Mzee alikohoa
Akacheka kidogo Akafukuza inzi
Kwa mkia wa ng'ombe
"Mnataka nini?"
"Hadithi!" Walijibu
"Hadithi gani?"
"Nzige! Nzige! Nzige!" ub. 2 (uk. 69)

Haya ni mazungumzo baina ya Mzee na watoto yanayotanguliza hadithi husika. Yanaonyesha namna mashairi andishi ya Kiswahili hutumia mazungumzo kuwasilisha ujumbe kishairi.

**Ngonjera**

Tofauti na mazungumzo, ngonjera ni majibizano ya kishairi kwa njia ya mdomo na ya papo kwa hapo (Mazrui na Syambo, 1992:56). Wahusika katika ngonjera husema jambo moja kwa ubeti mmoja na mwingine kujibu katika ubeti mwingine (Wamitila 2010:133). Katika diwani ya *Kichomi,* shairi '*Dakika kumi na tano za uzalendo*' lina ngonjera ambayo inahusisha wahusika kadhaa. Kwa mfano kuna majibizano baina ya Kijana na Mzee:

KIJANA: Mzee!
Mzee una habari, mambo yaliyotangazwa,
Ni lazima ufikiri, usikubali kupimwa,
Mambo sasa ni kikiri, Tanzania inasemwa,
Azimio limetajwa, tajiri wona hatari.

MZEE: Mwaka huu ni kilio, sisi hatuna mvua,
Tega vizuri sikio, huzuni itakuinua,
Nalo hilo azimio, latuletea mvua?
Sisi twataka mvua, tupate piga horio uk. 53

Katika dondoo hili wahusika wawili wanajibizana kuhusu Azimio la Arusha lililotangazwa. Mtunzi anaonyesha mwanya unaotenganisha vizazi viwili na thamani zao maishani. Matumizi ya majina ya kilakabu kama Mzee na Kijana yanaonyesha tofauti ya kiumri iliyopo kati yao. Mifano mingine katika shairi hili ni majibizano baina ya kijana, msichana na mama; msichana na kijana; tajiri na mzalendo; askari, tajiri na mzalendo.

Katika muhula wa Urasimi mpya, Diwani *ya Sauti ya Dhiki* inadhihirisha umbo la ngonjera. Shairi '*Mnazi: Vuta N'kuvute'* ni ngonjera mbali na kuwa na vipengele vya maigizo kwa sababu ya maelezo ya vitendo vya wahusika katika mtiririko wa mawazo ya mtunzi katika shairi. Maelezo ya mwandishi kuhusu kwa mfano mahala walipo wahusika (Alii, juu ya mnazi na Badi chini ya mnazi) yanaonyesha utendaji katika ngonjera hii. Shairi '*Kutendana'* (uk.89) pia ni ngonjera baina ya mwanamume na mwanamke.

Mifano hii inaonyesha namna umbo la ngonjera ingawa kipera cha mashairi simulizi hudhihirika katika Mashairi andishi ya Kiswahili.

**Mawaidha**

Mawaidha ni maneno mazuri ya maonyo au mafunzo yenye mwongozo (M'Ngaruthi, 2008:185). Yanaweza kutolewa kupitia masimulizi, mashairi, nyimbo, methali na vipera vinginevyo kwani msingi wake ni maudhui. *Utenzi wa Fumo Liyongo,* ingawa ni mughani una vipengele vya mawaidha. Mwanawe Liyongo anapomuuliza nini kinachomuua, Liyongo anamshauri kuwa achukue tahadhari kwani huenda angehadaika kumuua babake na kujuta baadaye. Anasema:

Baba umehadaika
Wao kisa watakuteka
Na kuzifanya dhihaka
Kisa utaiyutia ub. 141

Kuiyuta kinyumeni
Hela baba hufaani?
Ni kweli nimezodhani
Na yangawa t'akwambiya ub 142

Methali inatumiwa katika ubeti 142 kusisitiza mawaidha haya. Mshororo 'Kuiyuta kinyumeni' katika lugha nathari 'Majuto huja kinyume' unawasilisha ujumbe wa methali 'Majuto ni mjukuu huja kinyume'.

Katika muhula wa usasa tungo kadhaa ni mawaidha. Katika *Diwani ya Kichomi*, Kezilahabi pia anatumia mawaidha. Katika shairi '*Ukucha wa umbwa'* mhusika mkuu hadithini anamshauri bintiye kabla ya kifo chake, anamuachia ukucha wa mbwa ambao kwake ni 'dawa ya ulimwengu' na kumshauri autunze. Baadaye anapokosa kuutunza anaangamia. Ukucha wa umbwa hapa unatumiwa kijazanda kuonyesha thamani za jamii ambazo hazifai kutupwa na vizazi vya baadaye. Kadhalika katika shairi '*Hadithi ya kitoto'* mhusika mkuu Kanana anashauriwa na mamake kurudi kwa mumewe baada ya kutoroka huko.

Ni dhahiri hapa kuwa umbo la mawaidha linafungamana na maudhui ambayo ndiyo yanayowezesha uainishaji wake. Umbo lingine la maigizo ni ngoma inayodhihirika katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* katika densi ya Mwao.

**Semi**

Semi ni fungu la tungo za fasihi fupifupi zenye matumizi ya taswira, tamathali na ishara kwa mapana (Wamitila, 2010:135) Zinajumuisha methali, vitendawili, mafumbo, tanakali sauti, lakabu misimu na chemshabongo. Maumbo yote sita ya semi yalidhihirika. Semi nyingi zilionekana kutumika katika muhula wa Urasimi mpya ambapo Abdilatif Abdalla anaonekana kuegemea zaidi maumbo ya semi kuliko maumbo mengine.

**Mafumbo na Vitendawili**

Mafumbo ni kauli ambazo huficha maana fulani (Wamitila, 2010:150). Ni maneno yasiyojulisha maana waziwazi na hivyo huhitaji kufafanuliwa (M'Ngaruthi, 2008:87). Katika makala hii mafumbo na vitendawili zimetumiwa kurejelea dhana sawa.

Kezilahabi katika *Kichomi* anatumia umbo hili katika mashairi mbalimbali. Katika shairi *'Jinamizi'* uk.1, mtunzi anasimulia ndoto ya kutisha. Ndoto hii ni fumbo linaloashiria utawala wa kimabavu unaoendelezwa na wakoloni na hatimaye kupatikana kwa uhuru. Katika fumbo hili, utawala wa chuma ni utawala wa kimabavu unaoendelezwa na wakoloni; watu weusi na weupe waliosimama mtumbwini wanawakilisha askari Wazungu na Waafrika waliokuwa vibaraka wa utawala wa kikoloni; Waafrika watawaliwa wanawakilishwa na samaki ambao hawana uhuru wa kufanya lolote hivyo hawafai kusikika wala kuonekana; mamba ni watawaliwa waasi wanaoongoza harakati za kuikomboa nchi yao.

Shairi '*Afrika na watu wake*' vilevile ni fumbo. Katika shairi hili mwandishi anazungumzia bara la Afrika na matatizo yake. Anaeleza kuhusu mgonjwa aliyelala kitandani na ambaye hawezi kutembea kwa sababu ya miiba iliyomo miguuni mwake. Bara la Afrika hapa linalinganishwa na mgonjwa kwa sababu ya matatizo yake ya kisiasa na kiuchumi. Matatizo haya kwa mujibu wa mtunzi yanafaa kusuluhishwa kabla ya kusababisha madhara mengi kisha tahadhari ichukuliwe ili kusije kukatokea matatizo hayo tena. Anadokeza kuwa matatizo ya kisiasa na ya kiuchumi yanahitaji ujasiri mwingi ili kutatuliwa.

Vilevile shairi *'Ukucha wa mbwa'* (uk. 25) ni fumbo. Katika shairi hili mtunzi anasimulia kisa cha mama mjane kipofu aliyemrithisha mwanawe Amini ukucha wa mbwa; Kitu chenye thamani kilichofaa kumsaidia pamoja na jamaa zake. Hata hivyo baada ya kusoma na kujitajirisha aliudunisha na kuuona kama kitu cha aibu. Aliuweka sandukuni nyumbani hadi baada ya kifo cha mama yake. Baada ya miaka mitano aliukumbuka na kuuona kitu cha aibu na kuutupa sakafuni. Baadaye unamkwaruza na kumuua. Wengine wote, wakeze na wanawe wanachomwa na kuuawa na huu ukucha wa mbwa. Katika beti mbili za mwisho, mtunzi analifumbua fumbo hili na kueleza kuwa huu ni ukucha wa jadi ulioporomoka kutoka Arusha na kupelekea wengi kutoroka na kufa. Katika beti mbili za mwisho anadai huu si ukucha bali ni hasira za mababu.

Beti hizi zinaashiria kuwa vizazi mbali mbali vya Afrika vinaangamia kwa sababu ya kuacha mila, desturi, mafunzo, maadili na thamani walizoachiwa na wahenga wao. Wamevionea aibu vito vya thamani na kuiga mila zisizowafaa.

Katika shairi *'Hadithi ya Kitoto'* (uk.42) vilevile Kezilahabi anatoa fumbo ambalo linafumbuliwa mwishoni mwa hadithi. Mhusika mkuu Kanana (mwanawe Wesema) anazaa mtoto wa pili nje ya ndoa na jirani aliyemvunjia heshima alipokwenda kukopa pesa. Mumewe anapotambua kuwa mtoto huyo anafanana na jirani, Kanana anaamua kumuua kwa kumporomoshea jiwe baada ya kumpeleka msituni. Anaanza kukimbia lakini anashikwa na jitu kali linalomkaba roho. Ingawa yeye hakuliona alisikia sauti. Anageuka mwehu baada ya siku kadhaa za kukimbia usiku na mchana kisa na maana kufukuzwa na jitu kali lenye kisu mkononi. Hatimaye anakufa baada ya miezi miwili. Fumbo hili linafumbuliwa katika ubeti wa mwisho unaosema:

Mimi na wajukuu wangu sasa
Tunajuwa kwamba, wanasiasa,
Ingawa waue, na wasichana mimba watoe,
Sauti ya haki, ipo daima kuwafukuza.
Nami sasa naamini, kwamba hadithi rahisi
Kama hii yaweza kuwa ngumu kwa watu wazima. (uk.47- 48)

Mashairi mengine yenye mafumbo ni '*Hadithi ya Mzee'* (uk.69) na '*Fasihi'* (uk. 14).

**Methali**

Utanzu mwingine wa semi uliotumika ni methali. King'ei & Ndalu (2008) wanasema methali ni usemi mfupi wenye maana pana na busara au hekima ulio na mizizi katika jamii fulani na unaoelimisha, kuasa au kukejeli watu au vitendo fulani kwa njia ya kufumba. Methali zimetumika katika mashairi anuwai.

Katika shairi '*Mnazi: vuta n' kuvute*' methali *mpiga ngumi ukuta huumiza mkonowe* imetumika. Maana ya methali hii ni kuwa mtu anayepambana na mwenye nguvu huumia. Hutumiwa kumnasihi na kumwonya mtu asishindane na mtu anayemzidi kwa kuwa akifanya hivyo ataishia kujiumiza mwenyewe. Badi ndugu aliye mnazini anatumia methali hii kumuonya Alii nduguye aliye chini ya mti. Kadhalika kuna methali '*Ni heri nusu ya shari kuliko shari kamili'* imetumika.

Katika shairi *'Chema Hakidumu'*(uk. 47), mwandishi anaeleza jinsi ambavyo kitu kizuri au mtu mwema anavyokosa maisha marefu. Mshairi katika utungo huu anatumia methali hii kujifariji baada ya kuondokewa na jamaa zake waliokuwa wakimfaa. Vilevile methali *Mwerevu hajinyoi* imetumika kama mada ya shairi. Inaonyesha kuwa ujanja wa mtu una mwisho wake. Methali hii pia hujitokeza kwa sura tofauti kuwa '*Mwerevu hajinyoi, akijinyoa hajitakati, akijitakata hujikatakata'*

Katika shairi '*Ah! Mwenzangu'* (uk.29), Methali mbili zimetumika. Methali '*Mmejigeuza pweza unajipalia makaa'* imetumika kama kibwagizo cha shairi ambacho ukwapi wake unabadilika. Kwa mfano katika beti tano za mwanzo kibwagizo kinachukua sura zifuatazo:

1. Ufanyayo ni ya pweza, kujipalia makaa
2. Sina budi kukwambiya, wajipalia makaa
3. Hili nakwambiya wazi, wajipaliya makaa
4. Ingawa hunacho kicho, wajipalia makaa
5. Nakwambiya nisikiya, wajipaliya makaa

Ujumbe wa shairi ni wosia ambao mtunzi anamuelekezea rafikiye. Mwishoni mwa utungo huu anamuonya kuwa asipozingatia wosia huo huenda atajuta. Hapo anatumia methali: '*Majuto ni mjukuu (mwishowe huja kinyume)'.* Hata hivyo katika shairi hili, methali hii haitajwi moja kwa moja (uk. 31). Kadhalika methali imetumika kwenye kichwa cha shairi '*La Mjini na La Shamba*' (uk.74). Shairi hili ni ngonjera baina ya wahusika wawili. Mada yake inatokana na methali '*Jogoo la shamba haliwiki mjini'*. Kwa vile methali hubainika katika sentensi mifano inayotolewa ni mishororo.

**Vitanzandimi**

Vitanzandimi ni vifungu vya maneno ambavyo huonyesha mchezo mkubwa wa maneno yanayokaribiana kimaana na kisauti (Wamitila, 2010:169). Shairi '*Kuno Kunena*' katika Diwani *ya Sauti ya Dhiki* limejengwa kwa vitanzandimi. Mtunzi analalamikia mateso anayopitia kutokana na kauli zake. Hivyo anashangazwa na hali ambayo huenda inamuelekeza katika unyamavu. Je, awache kuzungumza? Ufuatao ni ubeti wa kwanza:

Kuno kunena kwa nini, kukanikomeya kuno?
Kwani kunena kunani, kukashikwa kani vino?
Kani iso na kiini, na kuninuniya mno
Kanama nako kunena, kwaonekana ni kuwi

Katika shairi hili sauti zilizotumika kujenga takriri yenye kutatanisha ni sauti / k / na / n /.

Vile vile shairi '*Tendekezo'* ni shairi lenye ubeti mmoja lililojengwa kwa vitanzandimi:

Tendekezo tendekezo, nazo zikutendekeze
Ziongezee mtwazo, nawo uziandamize
Yupi mwenye haja nazo? Nazitwae 'sizisaze
Upendaye tendekezo, twaa zikakupoteze

Hapa takriri sauti /t/, /nd / na /z/ zimetumika kuzua hali ya utatanishi. Katika utungo huu, mtunzi anahimiza hali ya kutekeleza jambo iwapo mtu ana haja. Anaeleza kuwa katika kutekeleza mambo mja ajitolee ili kufikia malengo yake bali asitegemee maneno matupu kwani hayaleti fanaka. Vilevile shairi '*Kokoiko'* katika *Diwani ya Sauti ya dhiki* limejengwa kwa tanakali sauti.

Katika mifano hii tunapata tanakali sauti na vitanza ndimi ambavyo ni vipera vya semi vilivyoingizwa katika mashairi andishi.

### Mashairi Simulizi

Sifa katika ushairi simulizi ni kuwasilishwa kwake mbele ya hadhira. Nayo yanahusisha nyimbo na mashairi (Wamitila, 2010:104).

### Nyimbo na Mashairi

Nyimbo na mashairi yametumika katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Liyongo anamtuma kijakazi Sadda kwa mamake na kumwambia akanene kwa ushairi. Maneno yake yanajitokeza katika ubeti ufuatao:

Kanena kwa ushairi
Enenda kamukhubiri
Mama afanye tayari
Haya nimezokwambiya ub. 105

Nyimbo zingine ni zile zilizotajwa na mtunzi anapoeleza kuwa wakati ngoma zilipoandaliwa nyimbo pia ziliimbwa. Na kila zilipozidi nyimbo na ngoma ndivyo Liyongo alivyozidi kukeketa minyororo (ub.115).

Kadhalika kuna nyimbo za kishairi katika *Diwani ya Sauti ya Dhiki.* Kwa mujibu wa King'ei & Amata (2001), mashairi yenye mishororo mitatu pia huitwa nyimbo. Mashairi '*Yatakoma*', (uk. 28), '*Watiliye Pamba*' (uk. 61) na '*Muosheni*' (uk. 75) ni nyimbo kwa kuwa ni tathlitha, ufuatao ni ubeti wake wa kwanza wa shairi '*Yatakoma*':

Sitokuwanayo, dawamu daima
Dhiki nilonayo, iliyon'egema
Ta'wa mbali nayo, utuwe mtima.

Naye, Kezilahabi anatunga '*Wimbo wa Kunguni*' (uk.20) na '*Wimbo wa Mlevi'* (uk. 64). Kutokana na vichwa vya mashairi haya ni wazi kuwa tungo hizi ni nyimbo.

### Sifo

Kipera cha maghani pia kilidhihirika kupitia utanzu wa sifo. Katika diwani ya *Kichomi* shairi 'Dakika 15 za uzalendo' ni pembezi. Kezilahabi anawasifu mashujaa walioongoza harakati za kupigania uhuru. Kimsingi shairi hili ni ngojera lenye maigizo. Hata hivyo, baadhi ya beti za shairi zinaonyesha sifa za pembezi. Ufuatao ni ubeti wake wa kwanza:

Ninaanza na Bushiri, liyeongoza maasi,
Mkwawa wetu mahiri, Mhehe mwenye makasi,
Kinjeketile tumkiri, na maji yake halisi,
Mirambo mkata rasi, Mbuni mke shuhuri. uk.59

Katika shairi hili mtunzi anawasifu mashujaa waliopigania uhuru. Pembezi nyingine inadhihirika katika shairi '*Mkwawa*' (uk.59). Katika shairi hili Mkwawa anasifiwa kwa kulinganishwa na sime ya dhahabu kuonyesha thamani yake katika jamii.

## Hitimisho

Kwa ujumla maumbo simulizi huchukua nafasi kubwa katika mashairi andishi ya Kiswahili. Makala hii inathibitisha hoja kuu ya nadharia ya mwingiliano matini kuwa hakuna matini yoyote ya kifasihi inayoweza kujisimamia bila kutegemea matini nyingine. Kwa mujibu wa Kristeva (1978) katika Ingemark (2005) wasanii hawabuni matini kutokana na fikra zao ila hukusanya mawazo kutoka kwa matini zilizopo. Katika hali hii ushairi andishi unajitokeza kama utanzu changamano ambao humeza na kuyeyusha maumbo sahili kama vile hadithi, semi, maigizo na mashairi simulizi.

**Marejeleo**

Abedi, K. A. (1954). *Sheria za kutunga mashairi na Diwani ya Amri*. Dar es salaam: East African Literature Bureau.

Abdalla, A. (1973). *Sauti ya Dhiki*. Nairobi: Oxford University Press.

Ingemark, C. (2005). *The Genre of Trolls, The case of Finland-Swedish Folk Belief Tradition*. Finland: Abo Akademi University Press.

Keen, S. (2015). *Literary Criticism* https://books.google.com/books? Isbn = //37439599

Kezilahabi, E. (1974). *Kichomi*. Nairobi: Heineman publishers

Kijumwa, M. (1964). *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Katika Mulokozi M.M. (2002). *Tenzi Tatu za Kale*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Dar es Salaam.

Kingéi, K. & Kemoli, A. (2001). *Taaluma ya Ushairi*. Nairobi. Acacia Stantex Publishers.

Knappert, J. (1979). *Four Centuries of Swahili Verse. A Literary history and anthology.* London: Heinenman Educational Books.

Kristeva, J. (1969). *Desire in Language: Asemiotic Approach to Litrature and Art.* NewYork: Columbia University Press http://Wikipedia.org/wiki

Kombo, D. K. & Tromp L. A. D. (2006). *Proposal and Thesis Writing;An Introduction.* Nairobi: Paulines Publications Africa

M'Ngaruthi, T. K. (2008). *Fasihi Simulizi na Utamaduni*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundations.

Mnyampala, M. (1965). *Diwani ya Mnyampala*. Nairobi: East African Literature Bureau.

Mulokozi, M. & Kahigi, K. (1979). *Kunga za Ushairi*. Dar es Salaam: Tanzania Pulishing House.

Musokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: East African Educnl. Publishers.

Ngure, A. (2003). *Fasihi Simulizi Kwa Shule za Sekondari.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Njogu, K. & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Ntarangwi, M.(2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Rock Island: Augustana College.

Roberts, S. (1972). *Utenzi wa Vita vya Uhuru.* Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Syambo, K., & Mazrui, A. (1992). *Uchambuzi wa fasihi.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Wafula, M., & Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki Wa Fasihi.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K.W. (2010). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi.* Nairobi: Focus Publishers.